UONGOZI WA KIKRISTO

Uongozi wa KiKristo: Mpango wa Masomo

Maelezo mafupi

DARASA #1:

I. Utangulizi.
II. Uongozi wa KiKristo ni nini?
   A. Ainisho ya Uongozi wa KiKristo.
   B. Ufunguo kwa Uongozi wa KiKristo.
   C. Maelezo juu ya Uongozi.
   D. Maandiko juu ya Uongozi.
   E. Aina za Uongozi.

DARASA #2:

II. Uongozi wa KiKristo ni nini? (inaendelea).
   F. Sura za Uongozi.
   G. Karatasi ya Kazi juu ya Uongozi.
III. Lini na Wapi ya Uongozi wa KiKristo.
IV. Kwa nini Mungu Alichagua Watu Wengine Kuwa Waongozi?
   A. Utangulizi.

DARASA #3:

IV: Kwa nini Mungu Alichagua Watu Wengine Kuwa Waongozi? (inaendelea).
   B. Kiongozi ni Safi.
   C. Kiongozi ni Mnyenyekevu.
   D. Kiongozi ni Mtumishi.
   E. Kiongozi Humtafuta na Humfahamu Mungu.
   F. Hitimisho.
   G. Sifa Zingine za Kiongozi Mzuri.
   H. Njia za Kuboresha Uwezo Wako wa Uongozi.

DARASA #4:

V. Kwa namna gani tunaongoza?
   A. Uongozi Katika Kazi, Unyenyekevu na Mfano - Yn 13:1-17.
   B. Jinsi ya Kuwa Mkuu.
   C. Wafuasi Walikuwa na Ufahamivu ya Kimwili kwa Ukuu.

DARASA #5:

V. Kwa namna gani tunaongoza? (inaendelea)
   Mtazamo wa Kidunia Kuhusu Ukuu.
   Utahini.

UONGOZI WA KIKRISTO

Maelezo mafupi

Uongozi wa KiKristo: Mtihani

Maswali yenye uwezekano wa kupata alama 20

1) Jadili "ufunguo kwa uongozi wa KiKristo (uk. 4, 5).
2) Taja na kueleza aina tofauti 3 za uongozi na (jumlisha tendo, mtendwa, ojinsi maandiko ya rejeo ya Kristo, na inavyo onekana katika Mt 21) (uk. 10).
3) Tumia dhana ya majira ya kanisa kuonyesha jinsi aina mbalimbali za uongozi vinavyo takiwa kwa ajili ya kanisa. Jumlisha mjadala wa dhana ya wingi wa uongozi na jinsi viongozi wanapashwa kufanya kazi kwa pamoja. (uk12, 17).
4) Jibu swali "Ni nini kinacho ruhusiwa?...Je ni sawa kufanya hili...? Je ni sawa kufanya lile?" (uk. 28, 29).
5) Tumia Yohana 13:1-3 kueleza kiini cha notisha ya mbinu za uongozi wa Yesu. (uk. 43-45).
6) Eleza jinsi ya kuwa mkuu kuliko wote (uk. 50-51).

Maswali yenye uwezekano wa kupata alama 10

1) Toa ainisho wazi ya uongozi wa KiKristo (uk. 3, 4).
2) Eleza maana ya sentensi (msemwa) hii "Huwezi kumwongoza yeyote hadi wewe mwenyewe utakopokuwa unaelekea mahali fulani. " (uk. 6).
3) Kwa nini ni kweli kuwa Mungu anahitaji wa kiongozi zaidi kuliko vipaji/uwezo wake (uk. 8)?
4) Ainisha kanisa lenye mwelekeo wa kufaulu kwa kutaja mkazo wake na kwa kutoa mstari na neno lake la ufunguo (uk. 12).
5) Sura 4 na uongozi ni zipi na Ingili na aina za uongozi zipi zina ambatana na kila sura (uk. 17, 18)?
6) Jadili mamlaka ya kibiblia kuhusu kuzaa watoto ukitaja mstari kuonyesha ni nani mwenye mamlaka pamoja na mfano wa jinsi baadhi ya watu hujaribu kutumia vibaya mamlaka katika suala hili (uk. 24).
7) Kwa kutumia Mt 5:8 onyesha umuhimu wa usafi katika maisha ya kiongozi (uk. 27, 28).
8) Eleza kwa kifupi kiini cha tatizo katika maisha na huduma ya kiongozi ambacho huzaliwa na kukosa unyenyekevu.(uk. 32, 33).
9) Jadili jinsi gani "uwezo wa kuona" ni sifa ya kiongozi mzuri (uk. 38).
10) Je viongozi huzaliwa au huandaliwa? (uk. 39)?
11) Jibu swali: ukuu hapinsuwa vipi? Rejea Yoana 13 (uk. 47, 48).
12) Jadili kwa kifupi "siri" za uongozi mzuri (uk. 52).

UONGOZI WA KIKRISTO

Maelezo mafupi

I. Utangulizi.

Ufafanusi wa Mwandishi:

Kwenye bampa ya gari liliko kuwa mbele yangu ilikuwa imebandikwa kartasi yenye maneno yasemayo: "Mbona unanifuata? Nimepotea pia." Mwendo haumanishi husudi siku zote. Kwa hiyo tusifuate kundi kila wakati makundi yaliyo mengi hayajui yaendako!

Ndiyo maana mafunzo haya hayaitwi tu "Uongozi." Kunaviongozi wengi duniani na kwa jinsi hiyo makundi mengi) ambao hawajui waendako (Mt 15:14). Tunahitaji Uongozi wa KiKristo. Swali letu la kwanza ni: Uongozi wa KiKristo ni nini?

Tia mfano hapo kati:

II. Uongozi wa KiKristo?

A. Ainisho La Uongozi wa KiKristo.

1. Uongozi.

   a. Wazo kuu ni kuweza kuwashawishi wengine..

   b. Kuongoza ni kuelekeza au kuonyesha njia.

2. KiKristo.

   a. Wazo kuu ni mtu. Kristo. Yesu Kristo.

   b. MKristo ni mtu ambaye lengo lake ni Kristo. Yesu ndiye kitovu cha maisha yake.

UONGOZI WA KIKRISTO

Maelezo mafupi

3. Uongozi wa KiKristo.

   a. Uelekezaji unaolenga kwa Kristo.

   b. Uelekezaji kwa Kristo.

   c. Kuonyesha njia kwenda kwa Kristo.

Shabaa La Mazungumzo

MJadilie juu ya tofauti kati ya uongozi wa KiKristo na uongozi wa kidunia.

B. Ufunguo wa Uongozi wa KiKristo.

1. Ufunguo ni kumtoa mtu kutoka mahali walipo sasa ndani ya Kristo na kuwasogeza hatua moja karibu zaidi na yeye.

   a. Kumleta mtu karibu na Yesu ni kumleta mtu huyo karibu zaidi na ufalme wa Mungu. Kuna viongozi wengine ambao hufanya kinyume (angalia Mt 15:14 na Mt 23:13).

   b. Kuna dhanio mbili katika ufunguo:

      1) “Kumtoa mtu kutoka mahali walipo sasa ndani ya Kristo" - hili lina dhanio kuwa kiongozi anawafahamu watu. Anaweza kuongea na fulani na kujua kwa kiasi fulani mahali walipo. Ana hekima na uelewa.

Maelezo mafupi

2) "Hatua moja karibu zaidi" --- hili lina dhanio kuwa kiongozi si mtu mwenye fikira zilizo mbali sana na hali halisi.

   a) Hategemei kupata zaidi sana kutoka kwa watu. Ana subira huenda hatua kwa hatua. Yu tayari kungoja hadi tunda litakafo iva. Hajaribu kumfanya mKristo mpya kuwa kiongozi mara moja hajaribu kumsukuma mtu apande ngazi tatu kwa mara moja.

   b) Yuko tayari kuwaacha watu wakue. Amejengeka vya kutosha katika huduma yake mwenyewe kiasi cha kupenda kuona wenginine wakiingia na kushika nafasi za uongozi. Hachukulii kukwama katika maisha ya kondoo wake kuwa ndiyo njia ya kuweza kawadhiliti. Anapenda kuona watu wakiwa karibu zaidi na Kristo.

Shabaa La Mazungumzo

Ukitumia kielelezo ifuatayo rfasiria ufunguo kwa uongozi wa KiKristo.

Kondo wa Mungu mchungaji wetu



2. Kiongozi mKristo lazima awasaidie wa kondoo wake kukuwa karibu zaidi na Yesu.

   a. Kuhusu kondoo #1: Kiongozi wa KiKristo mzuri hujua kondoo wake alipo na humleta hatua moja karibu zaidi na Yesu.

   b. Kuhusu kondoo #2: Kiongozi KiKristo mbaya hujaribu kumsukuma kondoo kwa nguvu sana.

   c. Kuhusua kondoo #3: Kiongozi wa KiKristo mbaya anahisi anatishiwa. Anaogopa kondoo wakue mno. Huenda wasimhitaji tena. Anajaribu kuwazuia kondoo wasiendelee kukua.

Maelezo mafupi

Tia Hapo Mfano Wako:

Shabaa La Mazungumzo

Sisi kama vile viongozi, lazima tujue vipindi mbalimbali ya ukuzi ya watu tunaowaongoza. Mzungumzie njia bora zaidi ya kugundua kiasi cha ukuzi cha watu wako na jinsi ungelivyopenda kutendea kila kikundi kwa ukuzi wake namna ya tofauti.

C. Matamshi kuhusu uongozi.

1. Huwezi kumwongoza yeyote hadi hapo wewe mwenyewe utakapokuwa unaelekea mahali.

   a. Kiongozi huelekeza kwa kiongozi lazima afahamu uelekeo lazima afahamu aendako ili kuweza kuwaongoza wengine pia.

   b. Kiongozi lazima awe na uwezo wa kuona. Lazima aweze kutazama mbele.

   c. Kiongozi lazima awe mtu aliye jitoa. Lazima ajitoe kwa ajili ya malengo yake.

   d. Kiongozi lazima awe na nguvu. Lazima awe anasonga mbele. Si mvivu. Lazima ayafanya yale ambayo wengine hawako tayari kuya fanya.

UONGOZI WA KIKRISTO

Maelezo mafupi

2. Kiongozi wa KiKristo anauwezo wa pekee wa kukaa kichwa mawingu ni na miguu aridhini.

   a. Ni wa kiroho na kimatendo.

   b. Huishi na Mungu na binadamu pia.

   c. Si "mtakatifu" kiasi cha kuto husiana na watu.

   d. Hafanani sana na "mmoja wa hao miamba" hata yasahau mambo ya kimungu.

   e. Yumo ulimwenguni lakini si wa ulimwenge (Yohana 17:14-16).

   f. Yu mtakatifu wa Mungu. Wakati huohuo ni mtu halisi ya wazi kwa watu wake. Hujilinganisha na watu na watu pia wana weza kujilinganisha naye.

3. Ukibaki hatua moja mbele ya watu wako, wewe ni kiongozi. Ukibaki hatua kumi mbele ya watu wako, wewe ni mfia dini.

   a. Ndiyo, kiongozi lazima ajitokeze mbele. Hata hivyo lazima abaki karibu kiasi cha kutosha ili asitengwe na watu wake.

   b. Panaweza kuwepo utengano wa ki-umbo na utengano wa ki-itikadi.

   c. Kiongozi lazima abaki karibu na watu wake kwa ukingo wake na kwa ukingo wake mwenyewe.

Tia Mfano Wako Hapo:

UONGOZI WA KIKRISTO

Maelezo mafupi

Shabaa La Mazungumzo

Tumia wazo zilizotangulia kwa kuzungumzia uongozi wa KiKristo kwa utambalisho wa kiongozi:

1) Anayekuwa mfano mwenye anaendelea hadi timizo.
2) Mwenye kufunuliwa na mwenye kutia katika matendo.
3) Mwenye kuwa karibu zaidi na watu wake.

D. Naandiko Kuhusu Uongozi.

Shabaa La Mazungumzo

Uwezo gani (vipaji vya asili) kiongozi anapashwa kuwa nao? Mitazamo gani (sifa za ndani) kiongozi anapa (agalia Kutoka 18:21, Matendo ya Nitume 6:3-5, I Timotheo 3:1-7, Tito 1:5-9, 1 Petro 5:1-3).

1. Watu wengi hufikiri kuwa ili kuwa kiongozi ni lazima uwe na vipaji vya asili vingi (ni kweli kuwa kina kipaji cha uongozi— Rom 12:8).

   a. Hata hivyo, matakwa ya ki Biblia kwa ajili ya viongozi ni matakwa ya Roho.

   b. Ni tabi ya ndani kuliko uwezo.

2. Kwa Nini? Kwa sababu uongozi wa KiKristo hasa ni uongozi na Yesu kupitia kwa kiongozi aliye teuliwa Yesu hahitaji vipaji vyako vya asili (ingawa hakika atavitumia vikiwekwa chini ya ukuu wake). Anahitaji moyo wako kwamo atakapo ingia.

3. Viongozi wanahitaji za kubadilisha (Tabia za kuwa wa). Ndipo Yesu anaweza kuongoza kupitia kwao. Huu ni uongozi wa KiKristo.

UONGOZI WA KIKRISTO

Maelezo mafupi

Shabaa La Mazungumzo

Kamilisha mchoro ufuatayo kwa kujifunza hizo ibada 5 na kufikiri kita takwa je takwa hilini kipaji cha asili ambacho baadhi tu ya watu wanacho? Au ni tabia ya ndani ambayo mtu yeyote anaweza kuchagua kuwa nayo?

Uwezo (Vipaji vya asili)	Tabia ya ndani (Maamuzi ya moyo)
Kutoka 18:21	Watu Wanaoweza (Wahebrania=Watu wenyo nguvu za Uagilifu) Watu wanao mcha Mungu Watu wa kweli (Wahebrania=Ukweli) Watu wanaochukia pato la udanganyifu Watu wa sifa nzuri Watu waliojaa roho
Matendo ya Nit. 6:3-5	

UONGOZI WA KIKRISTO

Maelezo mafupi

E. Aina ya Uongozi.

1. Si kila kiongozi huongoza kwa njia ile ile. Kila kiongozi ana mtindo wake na nyanja zake za kukazia.

2. Viongozi tofauti watakuwa na vipaji tofauti na watakuwa na haiba tofauti.

3. Kwa kawaida, kuna aina tatu za uongozi.

   a. Kuna uongozi wa kifalme.

   b. Kuna uongozi wa kinabii.

   c. Kuna uongozi wa kikuhani.

   d. Aina hizi tatu za uongozi msingi wake ni ofisi tatu za Kristo: Mfalme, Nabii, na Kuhani.

Jifunze mchoro ufuatayo:

Aina Ya Uongozi	Tendo	Mtendewa	Ofisi Ya Kristo	Kama ilivyo katika Mt 2:11	Kama ilivyo katika Mt 21
Mfalme	Hugawa Madaraka	Madaraka ya kanisa	Yoh 12:13	Mungu	Mstari wa 9
Nabil	Huelekeza	Kazi ya kanisa	Matendo 3:22	Manemane	Mstari wa 11
Kuhani	Hueneza	Neema ya kanisa	Heb 5:6	Uvumba	Mstari wa 12

(Angalizo: Zahabu ilikuwa zawadi iliyostahili kwa mfalme. Manemane ilitumiwa katika taratibu za mazishi...Yesu kuhani baadaye anyetabiri juu ya kifo chake mwenyewe. Uvumba ulitumiwa na kuhani katika huduma za hekaluni).

4. Kristo hushika ofisi hizi zote tatu ni kiongozi mkamilifu. Uongozi wa binadamu kwa kawaida utatilia mkazo juu ya moja ya ofisi hizi..

   a. Kuna viongozi wanao lenga kwenye madaraka na enzi (ofisi ya kifalme).

   b. Kuna viongozi wengine ambao hulenga kwenye upeo na uelekeo (ofisi ya kinabii).

Maelezo mafupi

c. Viongozi wengine hulenga kwenye maisha halisi ya watu na neema ya Mungu ambayo inapatikana kwa watu hao.

1) Tunapo tumia neno "kuhani" hatulitumii katika maana ya ukatoliki wa Roma wala kwamba ukristo ni "ukuhani" wa waumini. Tunalitumia ziadi katika maana ya kuhani wa Agano la Kale ambaye alihuduma kwa miaba ya watu - huduma yake ilikuwa ya kimatendo sana kulingana na maisha ya watu.

2) Hili, leo katika Kanisa, linawakirishwa na aina ya uongozi unao lenga watu - Tunaweza kumwelezea kiongozi huyu kama mwenye "moyo wa Mchungaji."

5. Hapa tunahitaji kukazia mtu viwili:

a. Kwanza, lazima tuelewe kuwa viongozi hawa wa aina zote tatu ni muhimu kuwa nao katika kanisa.

1) Kanisa litakuwa na aina tofauti za huduma ambazo zitahitaji hizi aina tofauti za uongozi.

2) Kanisa pia litapitia mabadiliko (haya tutayaita "Majira ya Kanisa"). Kila majira ya kanisa yanahitaji aina tofauti ya uongozi kulingana na mkazo wake.

b. Pili, lazima tuelewe kuwa mtu yeyote si Kristo. Mtu yeyote hataweza kuwa mfalme, nabii na kuhani.

c. Baada ya kuunganisha vipengele hivi viwili tutaona ulazima wa wingi wa uongozi katika kanisa hili hufundishwa katika Agano Jipya. (Tutalisoma kwa ukaribu zaidi katika mafunzo yaitwayo "Serikali ya Kanisa."

Shabaa La Mazungumzo

Aina zote tatu za uongozi ni muhimu kwa sababu zote tatu zina hitajika. Fikiria na kujadili siri ya uongozi wa kanisa lenye hali mzuri (lenye afya): Viongozi wa aina tofauti hujifunza jinsi ya kufanya kazi pamoja kwa sababu wanaona kuwa jinsi kila mmoja anavyo mhitaji mwenzake.

UONGOZI WA KIKRISTO

Maelezo mafupi

6. Aina hizi tatu za uongozi lazima itumike vizuri zaidi wakati inatiliwa pamoja kama vile kikundi cha uongozi.

   a. Jifunza mchoro ufuatayo:

Aina au Majira Ya Kanisa	Nguvu	Madhara	Mtindowa Uongozi	Kazi inayo Kaziwa	Linganisho
Ushirikiano: Mkazo ni juu ya watu; Ushirika Neno: Uhusiano Mstari: Yohana 13:35	Unafunzil Jamii	Mtazamo wa ndani, Ubinafsi: Uwezekano wa kuridhika mno kila mmoja na mwenzake na kusahuu juu ya roho zilizo potea	Kikuhani: Lengo kwa watu; maamuzi ya kundi	Ushauri; Ziana; Shughuli zingine za kichungaji	Chama cha Jamil//Msimamizi Katika Jamii au familia/Baba
Mafanikio: Mkazo ni juu ya malengo; majukuma Neno: Upeo Mstari: Mithali 29:18	Kazi nzuri; Ufanisi Ukamilishaji wa kutosha	Uwezekano wa Kukosa hisia kuhusu mahitaji ya watu; shughuli nyingi	Kinabii: Lengo kwenye jukumu; huainisha maamuzi yanayo takiuwa kufanywa	Huelekeza njia ya kufuata; huweka malengo na mipango; huweka mwelekeo	Shughali iliyo fanikiwa
Madaraka: Mkazo ni juu ya mamlaka; mpangilio wa madaraka Neno: Utaratibu Mstari:: I Wakorinto 14:40	Hakuna kuyamba; mazingira yaliyo fafanuliwa vizuri na kudhibitiwa	Kutumia vibaya madaraka; si wazi kpokea mawazo mapya; uweze kano wa kutoreke bika	Kifalme: Lengo kwenye madaraka uwezo wa kuathiri maamuzi ya wengine	Endesha na kuongoza; weka orodha ya amri; gawa madaraka	Kiwanda/Msima-mizi au Jeshi/Jemadari

   b. Hapa tunaongelea juu ya mkazo na lengo.

      1) Hatusemi kuwa kiongozi wa kinabii hajali watu. Tunachosema ni kwamba anaelemea zaidi kwenye majukumu.

      2) Hatusemi kuwa kiongozi wa Ki-Kuhani hutembelea, hushauri na kufanya kazi ya kichungajitu, tunachosema ni kwamba shughuli hizi mara nyingi ndiyo lengo lake.

      3) Ndicho anachopenda kufanya na ndicho anaweza kufanya (hii ni njia nzuri ya kuanisha vipaji vyako. Unapenda kufanya nini? Unauwezo wa kufanya nini)?

Maelezo mafupi

c. Chini ya daraja za linganisho zimetolewa linganisho mbili kwa kila aina ya kanisa.

1) Linganisho la kwanza zaidi sana ni linganisho la kidunia. Linganisho hili linaelezea zaidi hali ya aina ya kanisa au kiongozi wakati maendeleo yake ya kiroho yamesimama.

2) Linganishola pili zaidi sana na linganisho la ki biblia. Linganisho hili linaelezea zaidi hali ya aina ya kanisa au kiongozi wakatiana maendeleo ya kiroho.

a) Katika Efeso 2:19 kanisa huitwa nyumba au familia.

b) Katika 1 Wakorintho 3:9 huitwa jengo.

c) Katika 2 Timotheo 2:3-4 ni jeshi la askari.

d. Biblia hutumia malinganisho yote haya.

1) Mkazo juu ya mahusiano, mkazo juu ya upeo, na mkazo juu ya taratibu na mpango yote ni tofauti kabisa.

2) Aidha yote ni muhimu sana. Sura hizi zote za kanisa na uongozi wake ni lazima ziwepo kwa kiwango fulani wakati wote katika kila kanisa.

3) Hata hivyo kila kanisa litakuwa na mkazo wake kwa nyakati fulani za uhai wake.

4) Haya tunaweza kuyaita majira ya kanisa.

5) Tunaweza kuzungumzia juu ya kanisa kuwa na aina fulani ya "hali ya hewa."

Shabaa La Muzungumzo

Viongozi wengi wa kanisa wapenda zaidi kujenga uwingi wa uongozi wao toka mfano wa Waefeso 4:11-12 (pamoja na timu ya uongozi yenye kuweka ndani, Nabii, Mweneza Injili, Kasisi na Mwalimu). Zungumzo mafanano mbalimbali katika mifano hizi. Ufunguo ya lazima ni mifano miwili haya yanaomba timu au uwingi wa viongozi.

Maelezo mafupi

e. Hali ya hewa ya kanisa hubadilika, vipaji vya kiongozi havibadiliki.

1) Sasa ita kuwaje kama yupo kiongozi mmoja tu?

a) Kanisa itaumia.

b) Litahitaji aini tofauti ya vongozi kulingana na majira yake ya wakati huo.

2) Hapa tena tunaona umuhimu wa uwingi wa uongozi. Kama huu upo katika kanisa basi kanisa, liko tayari kukabili aina yote ya mabadiliko ya hali ya hewa.

Shabaa La Mazungumzo

Jifunze mchoro huu. Kuendeleza mjadala na mafumizi ya dhana zilizo tangulia.



7. Vangalizi juu ya majira ya kanisa na hali za uongozi (vyumba vya kazi).

a. Mungu aliyaumba majira. Huendelea katika mzunguko wa asili.

1) Majira ya baridi kali huendelea hadi majira ya uvuguvugu.

2) Majira ya uvuguvugu huendelea hadi majira ya joto.

3) Majira ya joto huendelea hadi maira ya baridi kali.

Maelezo mafupi

4) Majira ya baridi huendelea badi majira ya baridi kali na muzunguko huanza tena.

5) Kingetokea nini kama majira ya uvuguvugu ya singezika? Pasingekuwa na maisha mapya.

6) Majira ya baridi kali ni ya lazima. Ni muhimu kwa kila kitu kife. Ardhi hupumzika.

b. Hali kadhalika katika majira ya kanisa.

1) Linahitaji kuruhusu upeo na kazi za zamani kufa.

a) Linahitaji kuruhusu upeo na kazi za zamani kufa.

b) Linahitaji muda wa uponyaji wa ndani.

c) Linahitaji wakati wa kucheza kwenye theluji pamoja na wengine.

d) Linahitaji mkazo kwenye huduma ya kikuhani.

2) Hata hivyo, hufikia hatua ya wakati wa maisha mapya.

a) Ni wakati wa kuja kwa majira ya uvuguvugu.

b) Vitu lazima vianze kukua tena.

c) Watu wanahitaji kuamka.

d) Uongozi wa aina gani utakaowashitua waamke? Uongozi wa aina gani utawapa changa moto kuelekea kwenye malengo mapya? Utakuwa uongozi wa kikuhani? Hapana!

e) Ni wakati wa kuhazia uongozi wa kinabii.

f) Kanisa lazima litoke kwenye hali ya hewa ya udugu hadi kwenye hali ya hewa ya mafanikio, kama vile kipindi cha baridi kali kinavyo badilika hadi kipindi cha vuguvugu.

Maelezo mafupi

3) Lakini hutokea nini kama kipindi cha vuguvugu kisiingeisha?
   a) Ardhi itaku ya msitu!

   b) Baada ya kufikia hatua fulani, ni lazima kipindi cha uvuguvugu kikipe nafasi kipindi cha joto.

   c) Ukuaji lazima uwekewe mpangilio. Maisha mapya lazima yapangiliwe. Ndicho kifanywacho na uthabiti wa kipindi cha joto.

   d) Huduma ya kinabii lazima iipishe huduma ya kifalme.

   e) Hali ya hewa hubadilika kutoka kwenye mafanikio kwenda kwenye madaraka.

   f) Malengo yaliyo fikiwa pamoja na huduma mpya vinapangwa. Madaraka yanagawanywa kulingana na majukumu mapya.

4) Lakini hutokea nini kama kipindi cha joto hakiishi?
   a) Kila kitu hukauka. Si-unafsi.

   b) Ni wakati wa kufa kwa muundo wa zamani na vitu kunafsishwa tena. Hali ya hewa inabadilika.

   c) Hali ya hewa ya madaraka sasa inakuwa hali ya hewa ya udugu.

   d) Huduma ya kifalme lazima iipishe huduma ya ukuhani. Kipindi cha baridi kali kimerudi!

5) Yote hii inachukuliwa kuwa kuma uwingi wa uongozi.

   a) Aina zote za viongozi ni muhimu katika kila majira kwa sababu aina zote za huduma zina jitokeza katika kila jira.

   b) Hata hivyo, aina ya uongozi ambayo itakazwa itakuwa ile ambayo ina ambatana na majira ya kanisa ya wakati huo.

   c) Mkazo huu hubadilika kwa sababu majira hubadilika. Yaani, mahitaji ya kanisa hubadilika.

Maelezo mafupi

6) Waongozi wa nguvu na wa kusita wana hitajiana.

a) Ni rahisi kuona kwamba makuhani wana wahitaji manabii kushitua yale waliyo yafanya yalale.

b) Mana bii wanawahitaji wafalme kuyapanga yale waliyo yapangua.

c) Wafalme wanawahitaji makuhani kunafsisha yale yaliyoyapanga.

d) Viongozi wa sura mbalimbali wanahitajiana. Ni kanisa lenye afya ambalo viongozi wake wanayaelewa na kuyatenda haya.

Shabaa La Mazungumzo

Zungumza juu ya mahitaji kwa uwingi wa uongozi kanisani.

F. Sura za Uongozi.

1. Soma Eze 1:5, 10, na Ufu 4:7.

a. Sura hizi nne zina wakilisha nini?

b. Labda tunaweza kujibu swali hili kwa kujibu swali jingine. Kwa nini kuna Injili nne.

c. Kuna Injili nne kwa sababu kuna aina tafauti za uongozi. Yesu ni mfalme. Ni nabii na ni kuhani. Katika haya yote hutenda kama mwanadamu.

1) Hapa tunazo Injili nne: Matayo (Mfalme); Marko (Kuhani); Yoane (Nabii); Luka (Mtu).

2) Hapa tunazo sura nne: Matayo (Simba); Marko (Ngombe dume); Yoane (Koho); Luka (Mtu).

UONGOZI WA KIKRISTO

Maelezo mafupi

2. Jifunze mchuro huu uone sura nne ya uongozi (hii ni mfano wa tafsiri linaloonyesha kama mifano haya hayatoki halisi kwa maneno ya Biblia).

Sura	Injili na olina ya kiongozi	Hali na Mkazo wa Injili	Jina la Yesu Litumiwalo Zaidi
Simba	Matayo: Mfalme	Injili hii iliandikwa kwa ajili ya wayahudi. Ina mlenga Yesu kama mfalme shujaa na masiha mshindi.	Mwana wa Daudi: Jina hili linalenga kwenye huduma ya kifalme ya Yesu. Anaonekano kama Simba wa Yuda.
Maksai	Marko: Kuhani	Injili fupi kiliko zote. Inatoa orodha ya matendo ya Yesu bila maoni ya ziada. Kwa nini? Inamlenga Yesu kama mtumishi maisha yake ni Huduma kwa watu.	Mwana wa Mungu: Mwana ni mtumishi (tazama Fil 2:22). Anawatumikia watu.
Mwana--damu	Luka: Chombo	Hii ni Injili kwa wote. Iliandikwa kwa ajili ya binadamu wote. Inalenga kwenye huruma ya Yesu kwa ajili ya mahitaji ya watu. Tunamwona Yesu aliye mwanadamu.	Mwana wa Adamu: Jinahili linalenga kwenye utu wa Kristo. Tunaona uungu katika umbo la mwanadamu. Yesu awa chombo kikamilifu.
Tai	Yoane: Nabii	Injili hii ni rahisi lakini ina kina kuliko zote. Ina inlenga Yesu kama Mungu-manadamu.	Neno la Mungu: Jina hili linalenga kwneye siri ya Kristo. Linalenga kwenye asili yake ya kinabii.

a. Kuma Injili nne kwa sababu kuma aina tatu tofauti za uongozi za kuelezea na aina moja ya chombo ambacho kupitia kwa hicho, zote hufanya kazi. Sura hizi nne katika Eze 1 na Ufu 4 zinawa kilisha ukweli huu.

1) Simba anawakilisha huduma ya kifalme.

2) Tai anawakilisha huduma ya kinabii.

3) Maksai (ambaye ni mpole lakini mwenye nguvu - mtumishi mwaminifu asiye na kigeugue - mtaratibu na mwenye subira) anawakilisha huduma ya ukuhani.

4) Mwanadamu anawakilisha chombo ambacho huduma hizi zote zinafanya kazi kupitia kwake.

b. Ili ziweze kufanya kazi kwa utimilifu na ukamilifu, kwa sasa, lazima zidhihirishwe kupitia chombo zaidi ya kimoja. Huu unaitwa uwingi wa uongozi.

UONGOZI WA KIKRISTO

Shabaa La Mazungumzo

Maelezo mafupi

Zungumza mafasiri na jibia maswali yoyote kuhusu sura za uongozi.

G. Karatasi ya kazi juu ya uongozi.

Mazoezi ya darasani:

(itumiwe kwa mazoezi nyumbani au kwa mazoezi ya darasani).

1. Taja aina tatu za uongozi ambazo zimekuwa muhimu zaidi katika uzoezi wako maishani. Elezea juu ya kila aina hizo.

   - Mahusiano gani yalijumlishwa katika mazingira?
   - Je ilikuwapo migongano? Elezea juu ya moja au mbili yake.
   - Ulikuwa na jukumu gani? Ulikuwa na mamlaka gani?
   - Sehemu yako ilikuwa ipi? (Kama baba, ndugu, rafiki, bosi, mtaalamu na vivi hivi).
   - Uzoezi mzuri ni nini?

2. Andika sentense kumi juu ya silika na utendaji wa uongozi ukianza na maneno, "Uongozi ni..." Kwa mfano:

   - Uongozi ni kuwaelekeza wengine kwenye lengo.
   - Uongozi ni kuwashawishi wengine kufanya kitu fulani.
   - Uongozi ni...

3. Andika sentense 10 juu ya silika na tabia za MKristo ukianza na maneno "MKristo ni..." Kwa mfano:

   - MKristo ni mfuasi wa Yesu.
   - MKristo ni yule aliye na uhusiano na Yesu.
   - MKristo ni...

Maelezo mafupi

4. Unganisha sentence moja kutoka ulizo #2 na moja kutoka ulizo #3 ili kuunda sentence 10 zinazo anza na maneno, "Kiongozi wa MKristo ni..." Kwa mfano:

- Kiongozi wa MKristo ni yule anaye waelekeza wengine kumfuata Yesu (2a imeumganishwa na 3a).
- Kionngozi wa MKristo ni yule anayeshawishi wengine waishi kwa ajili ya Kristo.
- Kiongozi wa MKristo ni...

Orodhesha vitatu ambavyo ndiyo uwezo wako mkubwa zaidi kama kiongozi.

Orodhesha vitatu ambavyo ndivyo udhaifu wako mkubwa zaidi kama kiongozi.

Je viongozi huzaliwa? Au viongozi huandaliwa? Eleza.

Shabaa La Mazungumzo

Tumia kurudi nyuma toka makaratiasi ya kazi kwa mazungumzo ya darasa na ugawanyo.

III. Lini na Wapi Uongozi wa KiKristo.

A. Lini tunaweza kupata nafasi ya kuwa kiongozi?

1. Jifunze 1 Tim 3:5. Zingalia mchoro ufuatao:

a. Nyumba ya Mungu inaweza kusimama badala ya kanisa la Mungu (Efe 2:19).

b. Katika kigriki neno "simamia" ni neno lile lile linalotumika kuelezea kazi ya viongozi wa kanisa (kwa mfano katika 1 Tim 5:17).

UONGOZI WA KIKRISTO

Maelezo mafupi

2. Hapa Paulo anasema, "kama huwezi kukitawala kilicho chako mwenyewe, utawezaje kukitawala kilicho cha Mungu?" Kama huwezi kufanya jambo dogo, kwa nini unataka kujaribu kufanya jambo kubwa?"

   a. Jifunze Lk 16:10.

   b. Tunaanzia wapi? Tunaanzia na ya msingi. Anza na familia yako. Uwe kiongozi mzuri na kile ambacho Mungu tayari amekupa na utapewa zaidi.

3. Tunaweza kujihakikisha kuwa viongozi wazuri. Uwezekano wa kuwa na uwezo unaweza kuonyeshwa na uwezo halisi katika mazingira yanayo fanana lakini yenye utata kidogo.

4. Tunaweza **kujizoeza** na **kukuza** uwezo wetu wa uongozi.

   a. "Aliye mwaninifu katika kidogo ni mwaminifu katika kingi." Kwa sababu kuwa mwaminifu katika kidogo huzaa uwezo wa kuwa mwaminifu katika kingi.

   b. Njia nzuri hukuzwa katika kutenda vitu vidogo au vitu vinavyo jirudia. Njia mbaya hukuza katika kutendo vitu vidogo au vitu vinavyo jirudia.

      1) Kwa njia moja au nyingine utakuza wezo wako ndani ya hayo ya kila siku, yanayojirudia na nyanja za kimsingi za maisha yako.

      2) Kama siongozi vizuri ndani ya nyumba (au katika nyanji zingine ambako Mungu amenipa mamlaka), sina sababu ya kuamini kuwa nitaongoza vizuri katika kanisa.

      3) Kama ninaongoza vizuri ndani ya nyumba basi ninaweza walao kuwa na hakika kwamba ninakuza stadi shihi kuweza kuongoza katika kanisa.

Maelezo mafupi

5. Lini utapata nafasi ya kuwa kiongozi? Sasa hivi! Mungu atakupa nafasi zaidi baada ya **kujizoeza** na **kujihakikisha** wewe mwenyewe.

Tia Mafafanusi Yako:

Shabaa La Mazungumzo

Dhani swali: Umengojea kuamshwa katika usimamizi na uwezo zaidi kabla huusika na tabia zimeombwa kuwa kiongozi, au umeendeleza tabia na ustadi katika desturi ya kikao chako? Kumbuka, chimbuko hii imetumia kwa kuongeza pimamaji ya uongozi. Zungumza.

B. Wapi tutatumia mwezo wa vongozi wetu?

1. Uongozi wangu unaanzia wapi? Na unakomea wapi?

2. Jifunze Rom 13:1.

   a) Mungu ana mamlaka juu ya mamlaka yote.

   b) Mungu ameweka amri mbalimbali za madaraka ambazo ni lazima zisivunjwe.

   .

UONGOZI WA KIKRISTO

Fasiri ya Mwandishi:

Kusudi la somo hili ni kuchochea mjadala. Sanasana sio kuundia sera ya umma, bali kuonyesha uwepo na umuhimu wa amri za mamlaka. Mungu ameziweka. Mwanadamu asijivunje. Niwajibu wa kiongozi wa KiKristo kufahamu mamlaka yake yanapo anzia na yanapoishia. Lazima tuwe wangalifu sana katika eneo hili.

Maelezo mafupi

Shabaa La Mazungumzo

Jifunze mchoro kwa ukurasa wa 24 keva kuendeleza mazungumzo na mpako yenye kurejea amri na mamlaka mbalimbali.

UONGOZI WA KIKRISTO

Maelezo mafupi

Mamlaka	Familia	Kanisa	Taifa
Kuzaa watoto	Mwa. 1:28 Mwa. 2:24 Zab. 127:3-5	Kanisa halikupewa mamlaka haya. Kwa hiyo, kwa mfano,, ni makosa kanisa kumjaribu kutumia mamlaka juu ya mpango wa uzazi wa majira.	Taifa halikupewa mamlaka haya. Kwa hiyo, kwa mfano, katika uchina, sheria inayo weka kwango cha idadi ya watoto ambacho mama anaweza kuzaa ni kinyume cha Biblia. Kinyume chake, sheria ya kiromania iliyo lazimisha akina mama kuzaa watoto ni inyume cha Biblia pia.
Kufundisha	Kumb. 4:9,10; Kumb. 6:4-9, 20-25; Mez. 6:20-23	Kumb. 10: 12,13 Kumb. 29:29	Hakuna mamlaka yaliyotolewa, isipokuwa katika nyanja mchsusi za serikali. Polisi na mafungo ya kijeshi ni mifano miwili(shule za "Tax-run" zinadoheza nini?)
Kutunza maskini, wahitaji, wajane na Yatima.	Kumb. 15:4-11	Kumb. 16:9-15 I Yn. 3:17 Yak. 1:27 Mt. 25:31-40	Hakuna mamlaka yaliyo tolewa (Mifumo ya jamii, ujamaa na ukoministi inadoheza nini?)
Kutoza Kodi	Hakuna	Hakuna. Ingawa kanisa kamwe hali iiti kodi, ukweli wa baadhi ya mifumo ya utoaji wa moja kwa kumi ni kwamba hiyo moja kwa kumi ni kodi (kwa mfano, kanisa linalolazimisha na kudai moja ya kumi kutoka kwa wahaiki wake).	I Sam. 8:14-18 Rom. 13:6,7 Lk. 20:20-26
Kurudi au kuadhibu	Fimbo: Nidhamu Mez. 13:24; Mez.. 29:15,17 Efe. 6:14 (Taifa linajatibu kuwaondolea wazazi mamlaka haya katika U.S.A.).	Fimbo: Nidhamu II Kor. 13:1, I Kor. 4:21, I Kor. 5:1-13 (Taifa linajaribu kuliondolea kanisa mamlaka haya katika U.S.A.)	Upanga: Hukumu Rom. 13:1-5 I Pet. 2:13-14 Law. 19:15 Kumb. 25:1-3 Kumb. 19:1-10
Kuua	Hakuna	Hakuna (misiba ya vita vya dini ilitokea kwa sababu ya kukosa velewa wa kipengele hike).	Mwa. 9:6 Kumb. 19:11-13 Kut. 21:12-14 Law. 24: 17,21 Rom. 13:4

UONGOZI WA KIKRISTO

Maelezo mafupi

IV. Kwa nini Mungu alichagua watu wengine kuwa viongozi?

Mafafanusi ya Mwandishi:

Tabia na mwenendo ya kiongozi nii kama saa kwenye uwanja wa ndege. Saa hiyo ni muhimu zaidi kuliko saa zetu za mkononi kwa sababu inarekebisha saa zetu kulingana na hiyo saa. Vivyo hivyo na tabia ya kiongozi. Watu wengi hujiwekea vipimo vya mienendo yao kulingana na mwendo wa kiongozi. Viongozi wana daraka mkubwa. Kwa nini Mungu huwachagua watu fulani kuwa viongozi? Jibu halipatikani nje ya mtu. Linapatikana ndani ya mtu.

Tia Mafafanusi Yako:

A. Utangulizi.

1. Samueli alikuwa anatafuta mfalme. Hakumfikiria Daudi. Alikuwa mdogo mno. Samueli alidhani angekuwa Eliabu. Eliabu alikuwa mrefu. Ndipo Mungo aliponena. Alimuambia Samueli kwamba huwa ha chagui viongozi kwa kufuata kilicho nje. Huchagua viongozi kwa kufuata kilicho ndani (1 Sam 16: 6, 7).

2. Watu huchagua viongozi kwa kufuata kilicho nje. Wanatafuta kilicho bora na kina chozidi. Watu huchagua walio nadhifu zaidi, wazuri zaidi, wepesi zaidi, wenye sauti kubwa zaidi au mjumwisho wa "zaidi" na zingine. Hata hivyo, mara nyingi hizi "zaidi" zina nguvu kwa inje lakini kwa ndani ni dhaifu.

UONGOZI WA KIKRISTO

Maelezo mafupi

Mafafanusi ya Mwandishi:

Ziko kama magari ya spoti ya bei nafuu. Yanaonekana maarufu lakini yanapondeka kwa urahisi.

Ziko kama nyumba iliyo jengwa juu ya mchanga (Mt 7:27). Zijapo mvua, pepo na mafuriko, nyumba hizi huanguka. Ilikuwa nzuri kwa nje lakini kwa ndani dhaifu. Mvua, Pepo na mafuriko ya maisha hujikusanya juu ya kiongozi sura nzuri tu.

Tia mafafanusi yako:

3. Kwa nini Mungu huwachagua watu fulani kuwa Viongozi? Ni tabia gani ambazo anatafuta ndani ya kiongozi? Tutaanza kujibu swali hili kwa kutumia ainisho lifuatalo:

   a. Kiongozi wa kibiblia ni MTUMISHI SAFI na MNYENYEKEVU anaye MTAFUTA na KUMJUA MUNGU.

   b. Kwa kweli kiongozi ni chombo ambacho kupitia kwa hicho, Mungu huwaongoza wengine. Tunaweza kufafanua ainisho letu kwa kutumia kielelezo cha tarumpeta.

UONGOZI WA KIKRISTO

Maelezo mafupi



1) Kiongozi ni chombo. Vongozi huanzia na kuishia kwa kumtafuta na kumjua Mungu.

   a) Kiongozi amtafutaye Mungu atamjua Mungu (Mez 8:17).

   b) Kiongozi amjuaye Mungu atamtafuta Mungu (Yn 10:4).

2) Kiongozi ni chombo ambacho kupitia kwa hicho Mungu huwaongoza wengine. Kwa hiyo neno la ufunguo ni "tupu."

   a) Kwanza, usafi huondosha kilicho hasi. Huandaa utupu.

   b) Pili, unyenyekevu huweka utupu.

   c) Tatu, utumishihutumia utupu kwa njia chanya. Huuelekeza utupu kwa Mungu na wengine.

B. Kiongozi ni safi.

1. Umihmu wa usafi katika maisha ya kiongozi.

   a. Ufunguo wa uongozi ni kumleta mtu hatua moja karibu zaidi na Yesu.

   b. Ufunguo wa kumleta mtu hatua moja karibu zaidi na Yesu ni kufahamu njia ya kupitia.

Maelezo mafupi

c. Ufunguo wa kujua njia ya kupitia ni kuona anachofanya Baba (Yn 5:19).

d. Ufunguo wa kuona Baba anachofanya ni kuwa safi (Mt 5:8).

Shabaa la Mazungumzo

Jifunze mchoro ufuatayo.

Kuwa msafi moyoni (Matayo 5:8)
↑
Kuona ambacho Baba anafanya (Yn. 5:19)
↑
Kujua njia ya kupitia
↑
Kumleta mtu hatua moja karibu zaidi na Yesu

2. Usafi katika mawazo na matendo.

a. Danieli ni mfano mzuri (Dan 1:8).

b. Kiongozi lazima asiwe na lawamu (1 Tim 3:2). Lazima asiwe na mawaa.

1) Kinacho ruhusiwa ni nini? Kisichoruhusiwa ni nini? (Hili ni swali ambalo kiongozi anapaswa kulijibu kwa ajili yake mwenyewe na kwa ajili ya wengine).

2) Jibu ni: Inategemea! Kuna kanuni za kibiblia ambazo zianweza kutuongoza kuelekea kwenye jibu katika kila hali. Leroy Eims huziita konuni za 6-8-10.[1]

a) 6 = 1 Kor 6:12: Kinafaa? Kinanitawala?

b) 8 = 1 Kor 8:12, 13: Kitawakwaza wengine?

c) 10 = 1 Kor 10:31: Kinamtukuza Mungu?

Shabaa la mazungumzo

Tumia mchoro ufuatao kukuza mjadala na matumizi kuhusu tabia inayostahili kwa kiongozi Mkristo.

UONGOZI WA KIKRISTO

	6		8	10
Swali ➔ Jibu linalopendeke zwa ⬇	Inafaa?	Kinanitawala?	Kitakwaza wengine?	Kinamtukuza Mungu?
Unaweza kufanya	Ndiyo	Hapana	Hapana	Ndiyo
Hapana! Usifanye	Hapana	Ndiyo	Ndiyo	Hapana
Angalia. Inaweza kuwa bora kukiepuka	Bila upande	Sipo sasa. Lakini inawezekana	Kinaweza kama siwi mwangalifu	Inategemea mtazamo wangu

Maelezo mafupi

Fasiri ya Mwandishi:

Katika eneo hili, hatuwezi kuamini tu bila kuuliza. Mara nyingi jibu litakuwa: Angalia. Kiongozi lazima ampe mtu changamoto kufanya uamuzi wake mwenyewe. Kiongozi lazima ajipe changamoto yeye mwenyewe kuka mbali na matatizo kadiri iwezekanavyo. Kama kuna mashaka, basi kongozi anapaswa kuyaepuka mazingira hayo. Lazima awashauri wengine kufanya hivyo.

Mazingira tofauti huwaathiri watu tofauti kwa njia tofauti. Watu tofauti wana uwezo tofauti wa kuathirika. Kwa hiyo, inawezekana kuwa hali au tendo ambalo lina manufaa kwa mtu mmoja linapaswa kuepukwa na mtu mwengine.

Shabaa la mazungumzo

Tumia mazingira au matendo yafuatayo kama vipengele vya mjadala na matumizi.

1. Je, ninaweza kunywa glasi ya mvinyo?
2. Je, ninaweza kutazama onyesho fulani la televisheni?
3. Je, ninaweza kucheza michezo ya mashindano?
4. Je, ninaweza kuingia kwenye bata kushuhudia walevi?
5. Je, ninaweza kunywa kahawa?
6. Je, ninaweza kuhudhuria tafrija ya arusi yenye pombe?

Kumbuka kufumia kanuni za 6-8-10. Kama jibu siyo wazi, basi inaweza kuwa vema zaidi kuepuka mazingira au tendo hilo. Zaidi sana itategemea jibu la kweli la swali: Kusudi langu ni nini? Kwa nini ninataka kufanya hili?

UONGOZI WA KIKRISTO

Maelezo mafupi

3. Usafi ni kuwa chombo kwa kusudi za Mungu.

   a. Katika mpango wa Mungu wa uongozi usafi ni lazima kwa sababu viongozi hawaongozi kwa ajili ya Mungu. Mungu anaongoza kupitia kwa viongozi.

   b. Hapa tunazungumzia "nadharia ya chombo." Mungu hufanyo kazi kupitia kwa watu wake.

      1) Kwa hiyo tunaweza kuongelea juu ya "uongozi wa kichombo." Usafi unahusiana kwa katibu na uongozi wa kichombo (2 Tim 2:21).

      2) Jifunze 2 Tim 2:16-22.

         a) "Ajitakasaye mwenyewe" (mstari 21) unazungumzia juu ya usafi (Jifunze somo hili na tofakati mistari 16, 19b, 22a).

         b) Mtu ajitakasaye mwenyewe "amejiandaa" kwa kila kazi njema. (Tafakari kielezo cha tarumpeta. Usafi "huandaa" utupu).

         c) Chombo anachotumia Mungu lazima kiwe safi ili Mungu aweze kukijaza.

         d) Si matengenezo yetu yatakayo amua kama tutatumiwa kwa heshima au si kwa heshima. Ni hali yetu ya usafi (1 Sam 16:7).

Maelezo mafupi

4. Usafi wa kujitoa.

   a. Maana halisi ya utakatifu ni "kutengwa." Hapa tunaweza kuzungumzia usafi kwa maana ya kujitoa, kuwekwa na uaminifu kwa Mungu. Kiongozi sharti awe na usafi wa aina hii.

      1) Samsoni hakuwa mfano wa usafi katika misingi ya mawazo na matendo.

      2) Lakini alikuwa mfano wa usafi katika misingi ya kujitoa na kujiweka sakf. Alikuwa amewekwa maki kwa Mungu (Amu 13).

         a) Mungu anaweza kufanya viongozi kutokana na watu wasio na ukamilifu mradi tu wawe wamejiweka wazi kwake.

         b) Upendo hufunika wingi wa dhambi (1 Pt 4:8). Kuweka wazi hufunika wingi wa kasoro na udhaifu wa tabia.

   b. Kwa maana nyingine, usafi wa kujitoa ni muhimu zaidi kuliko usafi wa mawazo na matendo. Anachotaka Mungu kutoka kwetu, kuliko kitu chochote kile, ni kujitoa kwetu kwake (1 Sik 28:9). Ndipo atakapo badili tabia yetu. Ndipo atakapo ongoza kupitia kwetu.

Shabaa la mazungumzo

Tumia wazo zilizotangulia kwa kuendeleza mazungumzo kuhusu usafi wa kiongozi na ujihe maswali yenye kuelekea jambo hilo.

UONGOZI WA KIKRISTO

Maelezo mafupi

C. Kiongozi ni mnyenyekevu.

1. Leroy Iems anasema, "Njia ya kufikia furalia kamili ya maisha ni kuyaondosha macho yetu kwenye uelekeo wetu wenyenwe na kuishi kwa ajili ya wengine. Kiongozi atastawi tu wakati akitembea katika dhamira hii."[2]

2. Unyenyekevu wa kiongozi sharti umuwezeshe kuangazia juu ya wengine. Sharti umuwezeshe kuelekeza macho kwa Mungu.

   a. Mungu hutumia viongozi. Ni rahisi sana kwa kiongozi kujitazama yeye mwenyewe wakati Mungu anatenda jambo kubwa kupitia kwake.

   b. Jifunze Dan 2:27-30.

      1) Danieli alipinga kishawishi hiki.

      2) Mungu alitenda miujiza kupitia kwa Danieli, Danieli alinyosha kidole kuelekea kwa Mungu.

   c. Kiongozi sharti atafakali maana ya Is 42:8.

3. Kukosa unyenyekevu kutazaa matatizo mawili ya kimsingi katika maisha na huduma ya kiongozi:

   a. Kutojua.

      1) Kiongozi hawezi kuthubutu kukaa katika hali ya kutojua. Hata hivyo, kiongozi ambaye si mnyenyekevu ni kiongozi ambaye hawezi kufundishwa. Hawezi kupokea ushauri kutokea kwa wengine. Hawezi kujifunza na hawezi kukuwa (fikiria Mez 11:14 na 15:22).

      2) Baada ya muda mfupi sana, uongozi wake utakosa maana.

Maelezo mafupi

b. Kutokuwa salama.

1) Kiburi humlazimisha kiongozi ajitazama yeye mwenyewe. Ana shauku juu ya jinsi anavyoonekana kwa wengine. Kila mara anaangalia kwenye kioo. Kwa vyovyote vile hatimaye huugua kwa kutaka makubwa. Hana uhakika wa yeye mwenyewe na nafasi yake. Anajiona si salama.

2) Baada ya muda mfupi sana, uongozi wake hautakuwa na maana.

3) Mara nyingi hisia zake za kutokuwa salama huwa na matokeo ya kujaribu kudhibiti kila kitu na kila mtu anaye mzunguka. Anaanza kuonea badala ya kuongoza.

4. Unyenyekevu utamdumisha kiongozi.

a. Bila unyenyekevu kiongozi hupagawa na mafanikio yake. Ataanza kufikiria mno juu yake mwenyewe. Uongozi wake utaharibiwa.

b. Kwa sababu hii Paulo anatoa matakwa ya viongozi yanayo patikana katika 1 Tim 3:6.

5. Mungu huwatumia wanyenyekevu (Isa 66:2). Kiongozi muhimu kuliko wote katika agano la kale alikuwa Musa. Alikuwa pia mnyenyekevu kuliko wote juu ya nchi (Hes 12:3).

Angalizo: Tutajifunza unyenyekevu wa musa katika somo la "Tabia ya Kikristo."

Tia mafafanusi yako:

UONGOZI WA KIKRISTO

Maelezo mafupi

Shabaa la mazungumzo

Tumia mawazo yaliopita kuzungumza juu ya uzuri wa unyenyekevu na ubaya wa kukosa unyenyekevu.

D. Kiongozi ni Mtumishi.

1. John Haggai anasema, "ni mtu yule tu anayejitiisha mwenyewe katika nafasi ya utumishi na kuruhusu Kristo aendelee kumimina nguvu zake ndani yake, ameandaliwa maksudi kwa kuweka msukumo maalum ndani ya kundi, ili kuliendesha kuelekea kwenye malengo yenye manufaa ya kudumu, ambayo yanakidhi matakwa halisi ya kundi."[3]

2. Hali ya kuwa na uwezo wa kiuongozi hutegemea moyo wa mtumishi (Mk 10:43, 44).

   a. Yesu, ambaye alikuwa kiongozi mkuu kuliko wote katika historia aliyaelezea maisha yake kwa kusema, "kwa maana Mwana wa Adam naye hakuja kutumikiwa, bali kutumika" (Mk 10:45).

   b. Uongozi wa kibiblia si chanzo. Ni tokeo. Ni tokeo la utumishi. Uongozi wa kidunia huonyesha mamlaka badala ya utumishi (Mk 10:42-44).

3. Judson Cornwall anatukumbusha kuwa "Mungu hana nia na ukuu wetu. Ana nia na kupatikana kwetu. Ndiyo, mkuu kuliko wote ni mtumishi. Hata hivyo mtumishi hawi mkuu. Ana fanya tu ukuu upatikane."[4]

   a. Hatujazi. Tunatoa kile tulichojazwa nacho.

   b. Sisi si vitu vijazavyo. Tu vyombo vinavyo jazwa.

   c. Sisi si chanzo. Sisi ni kifaa.

   d. Sisi si yale maji ya uzima. Sisi ni mito inayo yahifadhi ni kuyachukua hayo maji ya uzima kwenye nchi kavu na zenye kiu.

   e. Hapa tena tunazungumzia "theolojia ya chombo" (2 Kor 4:7).

Angalizo: Tutajifunza mada ya utumishi kwa ukamilifu zaidi katika somo la "serikali ya kanisa."

UONGOZI WA KIKRISTO

Shabaa la mazungumzo

Tumia mawazo ya hapo awali kuzungumia juu ya kuitwa kwa Mungu kwenye kiongozi kuwa mtumishi. Pia zungumza shida ulinopata ikiwa kiongozi sio mtumishi.

Maelezo mafupi

E. Kiongozi humtafuta na kumjua Mungu.

1. Hali ya kuwa na uwezo wa kiuongozi huanzia hapa. Huanza na amri kuu kuliko zote (Mt 22:37, 38).

2. Daudi, alitumia muda mwingi peke yake na Mungu akiwa kijana mchungaji wa kondoo. Hali hii ilimtayarisha kuwa kiongozi.

3. Mungu ndiye chanzo cha nguvu za kongozi. Ushirika na Mungu ndiyo ufunguo unao fungulia nguvu hizo.

4. Mungu hupata kiongozi anapompata mtu ambaye yuko tayari kutanguliza mbele katika maisha yake ushirika na Mungu. Mtu anaye elekeza maisha yake kwenye uhusiano wakaribu na Mungu ulio bayana na wakimatendo. Huu ndio u "Nani" wa uongozi. Kupitia kwa mtu wa aina hii Mungu:

   a. Atadhihuisha uwezo wake (hii ndiyo "vipi" ya uongozi).

   b. Atatoa maelekezo yake (hii ndiyo "Nini", "Lini", na "wapi" ya uongozi).

   c. Ataonyesha hekima yake (hii ndiyo "kwa nini" ya uongozi).

5. Kumtafuta na kumjua Mungu vimehusiana moja kwa moja na imani (Ebr 11:6) kiongozi lazima awe mtu wa imani.

Angalizo: Tutajifunza mada hii kwa ukamilifu katika somo la "Kumjua Mungu I na kumjua Mungu II." Tutajifunza imani katika somo la "Imani."

UONGOZI WA KIKRISTO

Maelezo mafupi

Tia mafafanusi yako:

Shabaa la mazungumzo

Tumia wazo zilizotangalia kwa kuzungumzia jinsi gani kuchukua muda pamoja na Mungu ni ya maana kwako wewe kongozi. Ujadilie matukio ya kongozi mwenye kuwa na kazi kupita kiasi hata kukosa muda wa kuongea na Mungu.

F. Hitimisho.

1. Upendo wa kiongozi kwa Bwana utazaa wivu kwa ajili ya Mungu. Upendo huu na wivu huu utaendelezwa hadi kwao anaowaongoza.

2. Kiongozi wa kibiblia ni safi, mnyenyekevu, mtumishi anaye mtafuta na kumjua Mungu.

   a. Bila shaka ainisho hili si kamili. Tunaweza kuongezea sifa nyingine nyingi zinazo elezea. Hata hivyo, vipengele hivi ni baadhi ya vile muhimu.

   b. Ndani ya ainisho hili kuna upendo.

      1) Usafi bila upendo ni kujifanya watakatifu.

      2) Unyenyekevu bila upendo ni unyenyekevu wa uwongo.

      3) Utumishi bila upendo hauna faida yoyote (1 Kor 13:3).

      4) Kumtafuta na kumjua Mungu bila upendo haina faida (1 Kor 13:2).

      5) Kwa hiyo, upendo sharti ujumulishe katika sifa hizi zote.

Maelezo mafupi

c. Kiongozi wa Kikristo lazima awe karibu na Mungu. Lazima ampende Bwana kwa moyo wake wote (Mt 22:37, 38).

d. Lazima awe karibu na hao anaowaongoza. Lazima ampende jirani yake kama nafsi yake (Mt 22:39).

3. Matumizi.

a. Ninawezaje kuwa safi zaidi? Ninawezaje kuwa Mnyenyekevu zaidi? Ninawezaje kuwa mtumishi zaidi? ninawezaje kumtafuta na kumjua Mungu zaidi?

b. Uwe dhahiri - fanya uamuzi wa kutenda kitu fulani. Ainisha lengo lako, weka malengo mahsusi, na weka mpango, sasa fanya!

Maelezo ya Mwandishi:

Tafuta wa kushirikiana naye katika maombi. Omba naye kila siku. Uwe na kipindi maalum wa kutubu dhambi wakati wa maombi. Kuhusu sana, lenga kwenye zambi za uchafu.

Omba kwa ajili ya unyenyekevu kila siku. Mwombe Mungu akuhukumu kwa ajili ya kiburi katika mawazo, maneno, matendo na utaratibu wa maisha yako. Mwombe aondoe kiburi na kuweka unyenyekevu.

Jitolee kumtumikia mtu fulani. Uwe dhahiri jaribu kuto weka mashariti.

Tengeneza mpango wa kujitoa kila siku jaribu kujipangia katiba ya kila siku kwa mzunguko wa vipindi vitatu vya ushirika na Bwana (asubui, mchana, na usiku). Omba soma Biblia. Msifu na kumwabudu. Taribu kupanga muda usiopungua saa moja kila siku.

UONGOZI WA KIKRISTO

Maelezo mafupi

G. Sifa zingine za kiongozi mzuri.

1. **Ushujaa** -- vitabu vingi juu ya uongozi wa Kikristo vinakazia kuwa ushujaa ni tabia muhimu ya uongozi mzuri (fikiria Tito 1:9-11).

2. **Akili** -- kuhusu sana katika eneo la uamuzi na upambanuaji mzuri (fikiria Gal 6:1). Tunaweza kujumlisha busara, utulivu, na hekima (kwa mfano: leta matatizo yako kwa Wakristo wachache wanaoaminika na kuheshimika. Usilete matatizo yako kwa kila mtu. Maneno mengi na washauri wengi hufanya matatizo yakue).

3. **Uoni**-- Ni uwezo wa kupanga mipanga na kuwa mbele ya watu. Kiongozi sharti awe na uoni (fikiria Methali 29:18).

   a. Sharti aweze kufanya mawasiliano na wengine kuhusu uoni kwa wakati unaofaa, kwa watu wanaotakiwa, na kwa njia inayofaa.

   b. Sharti aweze kutoa maelekezo ambayo yanatoka katika moyo wa Mungu.

   c. Pia, uoni utabaini matokeo ya tendo kabla halijatendeka kwa njia hii kiongozi mwenye uoni anaweza kuwalinda watu wake.

   d. Mwisho, lazima ieleweke kuwa uoni halisi una miguu, uoni bila matendo ni ndoto tu. Uoni + imani + nguvu = mwendo.

4. **Uanzishi** -- ni uwezo wa kuanza vitu vipya. Katika baadi ya utamaduni, uanzishi hufikiriwa kama kiburi. Hata hivyo, uongozi bila uanzishi matokeo yake ni kuchanganyikiwa, na kukosa utaratibu na uratibu (fikiria Jos 1:10-18).

5. **Kusikitikia na kuhurumia** -- ni uwezo wa kuelewa, na kuthamini, na kusaidia wengine katika matatizo yao. Mara nyingi viongozi bora ni wale waliowahi kupata maisha magumu. Kutokana na uzoefu wanaweza kuhusisha na matatizo ya wengine (fikiria Mt 9:36; Waebrania 4:15).

6. **Nguvu** -- hii inajumlisha sura ya matendo na kazi za utii. Viongozi sharti wawe na busara. Hakuna kitu kinachoitwa kiongozi mvivu! (fikiria Matendo ya mitume 16:9-12).

UONGOZI WA KIKRISTO

Shabaa la Mazungumzo

Tumia wazo zilizotangulia kwa kuanzisha mjadala na kuleta mifano ya hizi sifa za uongozi jinsi zinaonyeshwa waziwazi ao kwa njia kamili.

Maelezo mafupi

H. Njia za kuongeza na kukuza uwezo wako wa ungozi.

1. Viongozi huzaliwa au hufanywa?

   a. Viongozi huzaliwa katika maana kuwa uongozi ni wito kutoka kwa Mungu. Uongozi ni kipaji. Si watu wote ambao ni viongozi.

      1) Fikiria Warumi 12:8 - neno la kuyanani hapa ni "proisteemi," ambalo lina maanisha kusimamia, kuelekeza, kutawala, ao kuongoza.

      2) Ni neno lile lile la kiyunani ambalo limetumiwa katika 1 Thes 5:12; 1 Tim 3:4, 5, 12; na 1 Tim 5:17.

   b. Viongozi hufanywa katika maana kuwa uongozi ni uwezo ambao unahitaji kukuzwa (fikiria Mithali 1:5). Nafasi kubwa zaidi za uongozi huenda kwa wale ambao wako tayari kwa nafasi hizo.

Andika mfano wako:

Maelezo mafupi

2. Je, viongozi wanaweza kuwa tayari? Wanawezaje kukuza uwezo wao?

   a. Tabia ya ndani.

      1) Nuia (jitoe) kufanya jitihada kwa ajili ya ubora. Hali ya kuwa nusu-nusu haiwapi heshima Mungu au mwanadamu (fikiria 1 Kor 14:12).

      2) Uwe na tabia ya ndani yenye afya (jifunze Filipo 3:12).

         a) Fahamu kuwa nafasi kubwa zaidi ni nafasi kwa ajili ya kuboresha. Kama utakoma kujifunza, basi utakoma kuongoza.

            (1) Paulo alisema: "Si kwamba nimekwisha fikia." Alitambua na kukubali kuwa hakuwa mkamilifu.

            (2) Tabia hii ya ndani humwezesha kiongozi kuendelea kukua na kuwa bora.

            (3) Tabia hii ya ndani humkinga kiongozi na uharibifu wa kiburi.

         b) Ridhika tu na kilicho bora (fikiria Mt 5:48).

            (1) Paulo alisema, "Bali nakaza mwendo." Aliendelea kuelekeza macho yake kwenye ukamilifu.

            (2) Tabia hii ya ndani humwezesha kiongozi kuendelea kukua na kuwa bora.

            (3) Tabia hii ya ndani humkinga kiongozi na uharibifu wa kukata tamaa.

         c) Tabia hizi za ndani zina sawazishana ili kujenga tabia ya ndani yenye afya.

            (1) Ukiwa na kimoja bila kingine, utakuwa na tabia ya ndani isiyo na afya. Au utataka uache, au hutaweza kusema kuwa umekosea au umetenda kosa.

            (2) Paulo aliweza kusema kuwa hakuwa mkamilifu. Hata hivyo, hilo halikumzuia kufanya jitihada kufikia ukamilifu. Alikuwa na tabia ya ndani yenye afya.

UONGOZI WA KIKRISTO

Andika mfano wako:

Maelezo mafupi

b. Matendo.[7]

1) Andaa kikamilifu kwa kila tendo la utumishi - hata kama ni nyenyekevu kiasi gani (Lk 16:10).

2) Chunguza uwanja ambao umo. Soma vitabu na magazeti chunguza (kama vinapatikana).

3) Kuza vipaji vyako vya asili. Namna gani? (Mt 25:14-30).

4) Kuza mazoezi mazuri ya kufanya kazi. Uwe na ufasaha katika kujisomea Biblia na maombi. Ratibu muda wako. Usichelewe-chelewe (2 Tim 2:15).

5) Omba nasaha au mashauri, maelekezo, ushari, na kukosolewa kutoka kwa watu waliofaulu katika uwanja wako. Uwe mwanafunzi (Mit 13:10; Mit. 19:20; Mit. 1:5; Mt 11:29).

6) Mtazame kiongozi mzuri anapotenda jiulize: Nini kinamfanya awe wa manufaa? Hayachukuaje mazingira fulani? Anajihusisha vipi na watu?

7) Kaa chini ya kiongozi mzuri. Uwe mwanafunzi kazini (tazama, jifunze, fanya kazi).

8) Utumiaji wa muda wako na Mungu upewe kipaumbele.

UONGOZI WA KIKRISTO

Maelezo mafupi

Andika Mfano Wako:

Kusudi la Mazungumzo

Tumia wazo zilizotangulia kwa kujadilia jinsi gani viongozi huweza kukuza uwezo wao. Onyesha mifano jinsi mafunzo hiyi ni ya kweli hakika.

V. Tunaongozaje?

Mfano wa Mwandishi:

Jemadari mzaliwa wa Amerika Dwight Eisenhower alitumia kipande cha uzi ili kuonyesha jinsi ya kuongoza wengine. Huku amekiweka kipande cha uzi mezani, alisema: "Ukikivuta kitakufuata. Ukikisukuma hakita enda popote."

Vivyo hivyo na watu. Wanahitaji mfano wa kufuata (tazam Yoana 10:4 na Luka 22:25, 26).

Eisenhower alisema, "Huongozi watu kwa kuwagonga kichwani. Hilo ni shambulio, sio uongozi.

UONGOZI WA KIKRISTO

A. Uongozi Katika Kazi, Unyenyekevu, na Mfano - Yn 13:1-17.

Maelezo mafupi

1. Kwa kutumia Yn 13, tunaweza kuweka ainisho la kimsingi la "namna gani" tuongoze.

   a. Utumishi (tendo).

   b. Katika unyenyekevu (tabia ya ndani).

   c. Kwa mfano (barabara au namna au kiungo).

UTUMISHI katika	**UNYENYEKEVU** kwa	**MFANO**
Tendo	**Tabia Ya Ndani**	**Barabara**

2. Kwanza, tunataka tujifunze ile "namna gani" ao "sababu gani" ya ile "namna gani." Yaani kusudi ya mfano wa utumishi katika unyenyekevu. Nini kili mkusudisha Yesu kuongoza kwa njia hii?

   a. Upendo (jifunze Yn 13:1).

      1) Upendo uli mkusudisha Yesu kuosha miguu ya wanafunzi.

      2) Kina cha upendo ni wazi zaidi tunapo tambua hali ya mazingira. Yesu alifahumu kuwa angeuwawa karibuni. Hata hivyo, anasahau juu ya mahitaji yake mwenyewe ili kuweza kuelekea kwenye mahitaji ya wanafunzi. Wakati ambayo angeeleweka vema kwa kuwa na ubinafsi alitenda tendo lisilo na ubinafsi kuliko yote.

      3) Upendo ni nguvu yenye uwezo sana. Inaweza kutuwezesha kutumikia wengine katikati ya mazingira magumu kuliko yote. Upendo haushindwi kamwe (1 Kor 13:8).

Maelezo mafupi

b. Usalama (jifunze Yn 13:1-3).

1) Adui, mkubwa kuliko wote, wa utumishi ni hali ya kuwa sisalama. Watu ambao sisalama hawako tayari kutumikia wengine kwa sababu kutokuwa salama kwao huwalazimisha wajitazame wao wenyewe.

2) Ili kuwa huru kutumikia wengine sharti uwe na hakika wewe ni nani ndani ya Mungu. Sharti ufahamu kuwa unafahamu.

3) Yesu alikuwa huru kutumikia kwa sababu ya usalama wake ndani ya Mungu Baba. Alifahamu kuwa anafahamu! Alikuwa anafahamu nini?

a) "Yesu, hali akijua ya kawa saa yake imefika, atakayotoka katika ulimwengu kwenda kwa Baba" (Yn 13:1).

(1) Sharti tujue tuendako. Lazima tuwe salama katika wokovu wetu.

(2) Yesu alijua alikokuwa anaenda. Hapakuwa na shaka. Hivyo, alikuwa huru kutumikia wengine. Kutokuwa na usalama katika eneo hili, matokeo yake ni mwelekeo wa kujitumikia mwenyewe.

b) "Yesu hali akijua ya kuwa Baba amempa vyote mikononi mwake" (Yn 13:3a).

(1) Sharti tujue tuna nini katika Kristo sharti tujue faida ya kuwa mwana wa Mungu. Sharti tuwe salama katika yule tulimo ndani ya Kristo.

(2) Yesu alijua ambacho alikuwa amepewa. Hapakuwa na shaka. Hivyo alikuwa huru kutumikia wengine. Pasipo usalama huu utataka kujaribu kujinufaisha utajitumikia mwenyewe.

Maelezo mafupi

c) "Na (akijua) ya kuwa alitoka kwa Mungu, naye anakwenda kwa Mungu" (Yn 13:3b).

(1) Sharti tujue tunavyo husiana na Mungu. Sharti tuwe salama katika uhusiano wetu na Mungu.

(2) Yesu alijua alivyo kuwa anahusiana na Baba. Hapakuwa na shaka. Hivyo alikuwa huru kutumikia wengine. Watu ambao sisalama katika uhusiano wao na Mungu hawako salama na watu. Hawawezi kutumikia.

4) Kutokuwa salama kwetu kunatulazimisha tufikirie sisi wenyewe. Hali hii inazuia uwezo wetu wa kutumikia wengine. Usalama hutoa kusudi ya kutumikia. Usalama hutufanya huru kutumikia.

Mfano wa Mwandishi:

Tumia mfano ufuatao kama kielelezo cha kipengele hiki.

Mwanamke na wanaume wawili wamesimama kwenye kituo cha basi. Mwanamke ana mtoto mdogo kwenye mkono mmoja na kwenye mkono mwingine anakitabu kikubwa cha mfukuni. Mvua inanyesha.

Ghafla mtoto anaruka kutoka mikononi mwake na kukimbia kuvuka barabara. Mwanamke huyu sharti aweke chini kitabu chake cha mfukoni na kumkimbilia mtoto. Lakini chini pana unyevu.

Anamgeukia mwanamume wa kwanza na kumwomba amshikie kitabu chake (ni kitabu cha kianakike sana). Anakataa kukishika. Anamwomba mwanamme wa pili kukishika. Kwa furaha, anakiweka kwapani na anasubiri yule mwanamke arudi.

Mwanamme wa kwanza hakuweza kumtumikia yule mwanamke. Kwa nini? Kwa sababu hakuwa salama katika utu uzima wake. Hakuweza kuelekeza macho kwenye mahitaji ya yule mwanamke. Alikuwa anajitazama yeye mwenyewe. "Watu wengi wangenifikiria nini? Mtu fulani huenda akanione - jirani yangu, mkuu wangu wa kazi au yule msichana mzuri kwenye ile bahari ngambo ya barabara!" Yote haya matokeo yake ni yeye kushindwa kumtumikia.

Yule mwanamme wa pili angeweza kumtumikia yule mwanamke kwa nini? Kwa sababu alikuwa salama katika utu uzima wake. Aliweza kuelekeza macho yake kwenye mahitaji ya yule mwanamke kuwa salama kwake kulimwezesha kuwa huru kutumikia.

UONGOZI WA KIKRISTO

Maelezo mafupi

Shabaa la Mazungumzo

Jinsi gani tunapata ushindi juu ya ukosefu wa mapendo na usalama ndani mwetu, ukosefu yenye kutukataza au yenye kutuzuia tufanye utumishi katika unyenyekevu kwa mfano?

3. Sasa tunataka kujifunza ufananisho katika ainisho letu la namna ya kuongoza. Ni nini ufananisho wa mfano huu wa utumishi katika unyenyekevu?

   a. Tendo la uoshaji miguu ni alama ya msalaba (uongozi sharti uwe alama ya msalaba).

      1) Jumla ya habari katika tendo la uoshaji miguu ni kwamba Yesu anarudi kwa Mungu. Saa yake imewadia. Anaenda msalabani (Yn 13:3).

      2) Wakati akimuosha miguu Petro, Yesu alisema, "kama sitakuosha miguu, huna shirika na mimi" (Yn 13:8). Tunafahamu kwamba ni kazi ya msalaba ndiyo ituoshayo.

      3) Wakati akimwosha miguu Petro, Yesu alisema, "Nifanyalo wewe hujui sasa; lakini utalifahamu baadaye (Yn 13:7). Ni msalaba ndiyo wanafunzi walikuwa bado hawajafahamu.

   b. Kwa njia iyo hiyo, uongozi wa Kikristo unapashwa kuwa alama ya kielelezo cha msalaba. Uongozi unapaswa kuwa matokeo ya kifu cha unafsi. Utumishi wetu na uongozi wetu unapaswa kuwa udhihiriso wa nje wa kifo cha ndani ambacho tumejionea.

   c. F.B. Meyer alielewa kuwa utumishi wa tendo la uoshaji miguu (tendo kuu kuliko yote la utumishi katika unyenyekevu kwa mfanoyaani, tendo kuu kuliko yote katika uongozi). Alitoa tafsiri hii ya (Yn 13:4, 5).

      “Aliinuka kutoka kwenye kiti cha enzi, aliweka kando mavazi yake ya nuru ambayo alikuwa amevaa kama nguo zake za ukasisi, akachukua vazi hafifu la ubinadamu, na kulizungushia juu ya utu wake wa utukufu; alimwaga damu yake mwenyewe ndani ya bakuli la msalaba, na kujitoa mwenyewe kuosha mawaa mashafu ya uovu na hatia ya mwanadamu.”[5]

Maelezo mafupi

B. Jinsi ya kuwa mkuu kuliko wote (jinsi ya kuwa kiongozi - endelea katika Yn 13).

1. Yesu alikuwa mkuu kuliko wote kupitia katika kifo chake (jifunze Flp 2:5-11 na Lk 22:26).

2. Mfano wa utumishi katika unyenyekevu (uoshaji miguu) ulifanywa na Yesu ili kujibu maswali ya wanafunzi kuhusu nani alikuwa mkuu kuliko wote.

   a. Wanafunzi walionekana kuhangaika sana juu ya suali hili: Mt 20:25-28; Mk 9:33-37; Mk 10:35-45; Lk 9:46-48; na Lk 22:25-27.

   b. Mwisho, Yesu aliamua kujibu swali lao (jifunze Lk 22:25-27 na tazama jinsi linavyo oana na uoshaji miguu katika Yn 13:12).

   c. Nani mkuu kuliko wote? Yesu anajibu swali lao kwa ufasaha:

      1) Mimi ndiye mkuu kuliko wote (Yn 13:13).

      2) Ninawatumikia (Yn 13:14).

      3) Niigeni mimi (Yn 13:15).

      4) Mtumishi si mkuu kuliko bwana wake (mstari 16).

   d. Ni nani mkuu kuliko wote? Yesu ndiye mkuu kuliko wote. Wao si wakuu kuliko yeye.

↓	↓
Ninawatumikia	**Niigeni mimi**

Maelezo mafupi

1) Jibu ni wazi. Yesu ni mkuu kuliko wote. Kwa nini Yesu ndiye mkuu kulido wote (kiongozi)? Kwa kuwa anatumikia.

2) Jinsi gani wanafunzi wanaweza kuwa wakuu? Sharti wamuige yeye. Sharti watumikie. Hii ndiyo NAMNA GANI ya uongozi au ukuu.

e. Je ukuu unapimwa namnagani? Unapiniwa katikasentimita aupaundi au lita? La unapimwa katika unyenyekevu na utumishi. Yesu alimba mstari wakupima ukuu. Upimaji wa ukuu ni katika unyenyekevu ne utumishi.

Rula ya Kupima Ukuu :!

1	2	3	4	5	6	7	8	9	10	11	12	13	14	15	16	17	18	19

Upimaji = utumishi na unyenyekevu

Shabaa la Mazungumzo

Tumia wazo zilizotangulia kwa kuzungumza jinsi gani utumishi na unyenyekevu yametumiwa kwa kupima ukuu wa uongozi wetu. Nini inatupasa kuonyesha kwa kuangalia mwisho wetu kweli sawa kiongozi, kama kipimo chetu cha utumishi na unyenyekevu ni chini?

f. Ukuu ni dhana inayo tegemea.

1) Kwa bahati mbaya (kama wale wanafunzi) tunaelekea kuufanya utegemee watu wengine.

2) Tuanjilinganisha na wengine. Ndivyo wanafunzi walivyokuwa wakifanya.

3) Lakini, Yesu anaweka kujilinganisha kwa yeye badala ya kujilinganisha kwa wengine. Yesu anawapa wanafunzi changamoto kumtazama yeye tu. Tunapotumia hili kwa maisha yetu wenyewe:

a) Tunafunguliwa kutoka kwenye kifungo cha ushindani.

b) Tunapewa changamoto kubwa. Matokeo ni unyenyekevu.

UONGOZI WA KIKRISTO

Shabaa la Mazungumzo

Jifunze na zungumza mchoro ufuatao.

Ukuu ni ulinganisho

Tunajaribu kuulinganisha na wengine

Tunaishi kati kautumwa wa ushindani. Kila mara kuna walio bora kuliko sisi katika mambo fulani. Tunaweza kukatishwa tamaa kwa urahisi.

Hatuwezi kusema: Bali nakaza mwendo (Flp 3:12)

Tunaishi katika utumwa wa kiburi. Kila mara kuna walio wabaya zaidi kuliko sisi katika mambo fulani. Tunaweza kuwa na kiburi kwa urahisi.

Hatuwezi kusema: Siyo kwamba nimekwisha fikia (Flp 3:12)

Ukuu ni ulinganisho

Yesu anaulinganisha na yeye mwenyewe

Tukitolewe kutoka utumwa wa ushindani hatuwezi kushindana na Yesu! Hatukatishwi tamaa. Tuko huru!

Tunaweza kusema: Bali nakaza mwendo (Flp 3:12)

Tunaishi na kisia kubwa ya changamoto. Hatuwezi kuwa bora kuliko Yesu! Hatuna kiburi tu wanyenyekevu!

Tunaweza kusema: Siyo kwamba nimekwisha fikia (Flp 3:12)

Maelezo mafupi

C. Wanafunzi Waliuelewa ukuu Kitumia (uongozi.

1. Waliuainisha ukuu kwa misingi ya mamlaka.

2. Walifanya ukuu kuwa ulinganisho wa kila mmoja.

3. Yesu aliubadili uelewa huo na uelewa wa kimbinguni.

   a. Aliainisha ukuu kwa misingi ya utumishi.

   b. Aliufanya ukuu kuwa ulinganisho kwake mwenyewe.

4. Kuhusu nani mkuu Judson Cornwall asema, "Mungu hana nia na ukuu wetu. Ana nia na umanufua wetu tu. Ndiyo, mkuu kuliko wote ndiye mtumishi. Lakini hata hivyo mtumishi hawi mkuu, hufanya tu ukuu upatikane."[6]

UONGOZI WA KIKRISTO

Maelezo mafupi

5. Ni nani mkuu kuliko wote? (Yn 13:13).

   a. Yeye ni mkuu kuliko wote vipi? Huongoza vipi? Utumishi katika unyenyekevu kwa mfano (Yn 13:14, 15a).

   b. Tunawezaje kuwa wakuu? Tunaweza kuongoza vipi? Kwa kumuiga Yesu (Yn 13:15b).

   c. Tunawezaje kumuiga Yesu? Mtumishi si mkuu zaidi kuliko bwana wake (Yn 13:16).

      1) Zingatia ambavyo dhama hii inavyo elezewa katika Yn 13:20. Inaelezewa kwa misingi ya Yesu ndani Yetu. Hii inalingana na uelewa wa kibiblia wa kuhusu kumuiga Yesu.

      2) Hatuwezi kurudia kunakili yale ambayo Yesu alikwisha fanya. Kwa maana hii hatuwezi kumuiga Yesu.

      3) Uigaji wa kibiblia unahusu kumruhusu Kristo kuishi ndani Yetu (tazama mwanzo wa mafunzo "Kumjua Mungu II"). Hivyo, njia pekee ya kumuiga. Yesu, njia pekee ya kibiblia ya kuongoza wengine -- njia pekee ya kibiblia ya kuwa mkuu ni kuruhusu yule aliye mkuu kuishi ndani yako (Gal 2:20).

Shabaa la mazungumzo

Hapa lazima tuwe wangalifu kuhusu tofauti kati ya hali uwezekano wa ukuu na ukuu halisi. Jifunze mchoro ufuatao. Zungumza umbalimbali katikati ya mafundisho ya siri ya mashariki na ukristo wa kweli.

UONGOZI WA KIKRISTO

Maelezo mafupi

Uwezekano wa Ukuu

3 — 2 — 1 — Uwezekano wa ukuu

Kadri kifo kwa unafsi kinavyoongezeka, uwezekano wa ukuu huongezeka kwa sababu uwezekano wa kumruhusu aingie ndani yule aliye mkuu huongezeka (fikiria Mk 10:18).

3 — 2 — 1 — Kifo kwa unafsi

Ukuu Halisi

3 — 2 — 1 — Ukuu halisi

Kadri kifo kwa unafsi na kuishi kwa ajili ya Yesu kunavyo ongezeka, ukuu halisi huongezeka kwa sababu uhalisi wa kumruhusu kuingia ndani yeye pekee aliye mkuu huongezeka.

3 — 2 — 1 — Kifo kwa unafsi; kuishi kwa ajili ya Yesu

Tofauti kati ya uwezekano wa ukuu na ukuu halisi ni tofauti kati ya kujitoa kwa mtafuta mashariki na kujitoa kwa Mkristo.

Mtafuta Mungu wa mashariki hufa kwa unafsi ili kujidhihirisha mwenyewe. Mkristo aliyejitoa kufa kwa unafsi ili kumdhihirisha na kuishi kwa ajili ya Yesu.

D. Ufupisho.

1. Tunaongoza vipi? Tunaongoza kupitia kwenye utumishi katika unyenyekevu kwa mfano.

2. Tunapata motisha kutokana na upendo na usalama katika Mungu.

3. Uongozi wetu sharti uwe kielekezo cha msalaba.

4. Kiongozi (wa wakuu kuliko wote) ni mtumishi.

5. Ukuu hupimwa kwa utumishi na unyenyekevu.

6. Ukuu hulinganishwa kwa Yesu. Haulinganishwi kwa wengine.

7. Yesu ndiye Mkuu kuliko wote. Tukitaka kuwa wakuu sharti tumruhusu awe Mkuu kupitia kwetu. Kama tunataka kuongoza, sharti tumruhusu aongoze kupitia kwetu.

Maelezo mafupi

8. Mwisho, kumbuka hitimisho la Yesu kulingana na mambo haya: "Basi ikiwa mwaya jua haya mtakuwa na heri mkiyatenda." (Yn 13:17).

E. Nyongeza: Siri 12 za Uongozi Mzuri.[8]

1. Fahamu maendeleo katika uwanja wako (soma vitabu, magazeti, ongea na viongozi wengine).

2. Kila mara sikiliza panda zote za tatizo. Usichukue hatua kutokana na taarifa za mtu mmoja tu.

3. Usisaliti imani. Ikiwa mtu fulani atakuomba kuweka ujambo fulani kama siri na ukakubali, basi lazima utunze siri hiyo. Kama watu hawawezi kukuamini basi utumishi wako hautakuwa na maana.

4. Usiuzike unapo shindwa.

5. Jaribu kujadili tofauti kati ya watu. Uwe mpatanishi (Mt 5:9).

6. Zuia hasira zako.

7. Usifikiri sana juu yako mwenyewe. Baadi ya watu watapenda kukulipua kama puto. Uwe tayari kujicheka mwenyewe.

8. Usijaribu kuyakimbia matatizo yako (kushindwa, upinzani, malalamiko, ukosaji). Kumbuka: Matatizo hayatoweki. Hutatuliwa.

9. Usiruhusu tamaa ya kujinufaisha itawale uamuzi wako.

10. Onyesha heshima sawa kwa walio chini ya mamlaka yako kama wale walio juu yako ki mamlaka.

11 Kubali kuwajibika katika kushindwa na katika kufanikiwa.

12. Tafuta na kuandaa nafasi kwa ajili ya kuwakuza hao unao waongoza.

UONGOZI WA KIKRISTO

Uongozi wa Kikristo: Mwisho

Maelezo mafupi

[1]Leroy Eims, Kuwa Kiongozi Unayotamani (Wheaton: Victor Books, 1975), uk. 30. Mchoro umetegemezwa juu ya chanzo "6-8-10". Hutumiwa na ruhusa.

[2]Kile kile kilichotajwa, uk. 32.

[3]John Haggai, Ongoza (Waco: Word Books, 1986), uk. 71.

[4]Judson Cornwall, Umbo za Kiongozi Kwa Upande (Plainfield: Logos International, 1980), uk. 220.

[5]F.B. Meyer, Mapendo Sana (NY: Fleming H. Revell Co., 1988), uk. 18.

[6]Cornwall, uk. 210.

[7]Imetengenezwa toka masomo ya darasa, Chanzo za Uongozi, Dr. Dan Hedges, Regent University, 1987.

[8]Kile kile kilichotangulia.

UONGOZI WA KIKRISTO

Maelezo mafupi